

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
Tarehe 7 Oktoba 2006**

**Waliohudhuria**

Elaine Baker  
Israel Kiyame  
Juma Ali Salehe Jongo  
Kibwana Mohammad Msiga  
Maurus Malikita

**Wageni**

Leon Mlambo	AALOCOM
Prosper Nyaki	AALOCOM
Selemani Majembele	AALOCOM

Tulizungumza kuhusu jinsi Serekali wanavyogonga biashara ndogo ndogo, hata zile ambazo zipo maeneo ya nyumba za watu na siyo kwenye barabara kuu, na matokeo kwa maisha ya watu wengi. Kioski za fundi za baisikeli zimegongwa pia na hii inasababisha iwe ngumu kupata huduma ya fundi baisikeli au kutengeneza pancha.

Prosper alipitia ajenda ya mkutano wa mwisho kuhusu msafara wa baisikeli. Wanachama wa UWABA walisema wameweka mabango na wamesambaza vipeperushi kwenye maeneo mbali mbali na wataendelea kufanya hivi wiki ijayo. AALOCOM wametafuta matangazo ya gazeti na watatafuta matangaza ya redio. Pia wamepata naibu meya kuwa mgeni rasmi.

Njia ya msafara ulibadilishwa iwe Karimjee – Ocean Road – Salender Bridge – Barabara ya Ali Hassan Mwinyi– Morocco – Barabara ya Kawawa– Magomeni – Lumumba St – Samora Avenue na kurudi tena Karimjee. Tutakuwa na mapumziko mfupi Kinondoni ile washiriki wanye maji. Msafara utaendelea pole pole ile watu wasibaki nyuma.

AALOCOM wametafuta maji na soda kuwapa washiriki. Walipendekeza gari ifuate msafara kwa ajili ya msaada wa kwanza na tulikubali kama baisikeli zionekane zaidi kuliko gari. Mtu wa msaada wa kwanza awe ndani ya gari.

AALOCOM pia wametafuta waandishi wa habari wa TV wawe Karimjee.

Tulizungumza kuhusu utoaji wa jumbe za msafara. UWABA tutatengeza mabango ya jumbe za baisikeli, megaphones kwa watu kwenye maguta kutoa jumbe na muziki.

Ratiba itaanza na maneno ya ufunguzi halafu msafara utanza. Wakati washiriki wanarudi Karimjee mwisho wa msafara, watapewa tiketi ya bahati nasibu – kila mtu apate tiketi moja tu na viongozi wasichukue tiketi. Tutakuwa na hotuba kutoka mgeni rasmi na kila shirika tutakuwa na nafasi kutoa maneno mafupi kuhusu mambo ya baisikeli na shirika lao. Mwisho mgeni rasmi atachukua tiketi za bahati nasibu na baisikeli tano za California zitatolewa.

Tulikubali kutana tena saa kumi mchana ijumaa kabla ya msafara kuhakikisha kila kitu ni sawa.